**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA WAZIRI MKUU**

**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

# MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE ZA SEKONDARI ZA SERIKALI TANZANIA

**Juni, 2026**

**Dodoma**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA WAZIRI MKUU – TAMISEMI**

**Mkuu wa Shule: 0786763078**
**Makamu mkuu wa shule 0685128372**
**Mwandamizi Taaluma: 0682247054**

**Shule ya Sekondari Kitomanga,**
**S.L.P. 464,**
**Lindi.**
**15/05/2026.**

**Mzazi/Mlezi wa Mwanafunzi …………………………………………………………………….**

YAH**: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE YA SEKONDARI KITOMANGA ILIYOPO HALMASHAURI YA MANISPAA YA LINDI MKOA WA LINDI MWAKA …………………**

Nafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na Kidato cha Tano katika Shule hii mwaka ……………. na atasoma tahasusi ya ……………………….

Shule ya Sekondari Kitomanga ipo katika Halmashauri ya Manispaa ya Lindi umbali wa km 55 kutoka Lindi Mjini. Shule ipo pembezoni mwa barabara kuu ya Lindi - Dar es Salaam katika kijiji cha Kitomanga.

Kwa wanaotoka Dar es Salaam panda magari yanayoenda Lindi / Mtwara shuka kijiji cha Kitomanga. Aidha, kwa wanaotoka upande wa Mtwara / Lindi panda magari yanayoelekea Dar es Salaam / Kilwa kisha shuka kijiji cha Kitomanga. Nauli kutoka kijijini hadi shuleni ni TSh. 1000/-. ***Kutokea pande zote (Lindi au Dsm) unaweza kuomba msaada ushukie shuleni moja kwa moja.***

Muhula wa Masomo unaanza tarehe **………………**, hivyo mwanafunzi anatakiwa kuripoti shuleni tarehe **…………..** Mwisho wa kuripoti ni tarehe…………………

Blaher

**BAHIA TAHER ABUBAKAR**
MKUU WA SHULE

MKUU WA SHULE
KITOMANGA SEKONDARI
LINDI

## 1.0 MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA

### 1.1 WAVULANA

**i. SARE YA SHULE**

i. Suruali mbili zisizobana na zenye urefu wa heshima (mshono wa kawaida kadri ya vipimo, zenye rinda mbili kila upande,upana wa chini wa suruali usipungue inch 7.5)

ii. zingatia picha ya kitambaa kwa sare za darasani kama ilivyoambatanishwa katika fomu hii.

iii. Mashati mawili meupe (2) mikono mirefu (tetron)

iv. Soksi jozi mbili rangi nyeupe (**white**) za shule

v. Viatu vyeusi vya shule vya kufunga kamba vyenye visigino vifupi

vi. Mkanda mweusi wa ngozi wa kuvalia suruali

vii. Sare ya michezo bukta moja rangi ya blue, fulana moja rangi ya blue ambayo ni jezi ya timu ya **Chelsea** ya msimu wa 2025/2026 angalia kwenye picha iliyoambatanishwa.

viii. Raba za michezo (**daruga/au Njumu)** kwa ajili ya mazoezi.

ix. Sweta moja rangi ya kijivu iliyokolea lisilokua na mistari (white strips).

x. T-shirt ya shule zinapatika shuleni kwa shiling **16,000/= kwa atakayehitaji**

xi. Nguo za kushindia (shamba dress) suruali mbili **Damu ya Mzee**

xi. Track suit moja rangi ya **DARK BLUE** yenye white strip (imeambatanishwa)

xii. T shirt kuanzia moja rangi ya **KIJIVU YENYE KOLA** kwa ajili ya kushindia.

**ii. MAHITAJI MENGINE MUHIMU KWA WAVULANA**

i. Blanket moja futi 3x6 (kwa atakae hitaji kutokana na hali ya hewa ya joto)

ii. Shuka mbili za rangi ya blue bahari

iii. Nguo za ndani za kutosha

iv. Vest za rangi nyeupe

### 1.2 WASICHNA

**A. SARE YA SHULE**

i. Sketi mbili kwa muonekano ufuatao;
   - Sketi ndefu kutoka kwenye kisigino mpaka kwenye pindo la sketi zisizidi sentimeta 18 au inchi 7.5 (**urefu wake ufike kwenye kifundo cha mguu**)
   - Sketi zisiwe na mkanda mpana, upana wa mkanda (belti) usiozidi sentimeta 5 au inchi 1.5
   - Rangi ya kitambaa imeambatanishwa katika fomu hii.
   - Mshono wa sketi ni ***LINDA BOKSI*** moja kubwa katikati/ mbele na linda ndogo mbili pembezoni mwa linda kubwa.

ii. Mashati mawili meupe (2) ya mikono mirefu kwa wasiovaa hijabu.

iii. Kwa wanaovaa hijabu; Blauzi nyeupe (**NUSU KANZU**) isivuke magoti na lazima ifunike makalio na iwe ya mikono mirefu

Hijabu au Juba nyeupe na sio mtandio isiwe na urembo wowote pia isiwe na urembo wa lesi, inayofunika mikono

iv. Tshirt zenye nembo ya shule zinazopatika shuleni kwa Tshs. **16000/=**

v. Soksi rangi nyeupe (**white**) za shule jozi mbili ndefu

vi. Raba jozi moja kwa ajili ya mazoezi

vii. Sare ya michezo fulana moja rangi ya **blue** ambayo ni jezi ya timu ya **Madrid** ya msimu wa 2025/2026 angalia kwenye picha iliyambatanishwa.

viii. Truck suit **DARK BLUE** yenye white strips kwa ajili ya maandalizi ya jioni

ix. Sweta moja ya kijivu iliyokolea lisilokua na mistari (white strips).

x. Magauni mawili (Shamba dress) rangi ya **MAROON** (damu ya mzee). Mshono wa **SOLO** yenye mikono mirefu na juba la **maroon** kwa wanaovaa hijabu na mikono mifupi kwa wasiovaa hijabu, liwe gauni lililoshuka hadi chini na lisilobana.

**A. MAHITAJI MENGINE MUHIMU KWA WASICHANA**

i. Shuka mbili rangi pinki.
ii. Taulo za kike za kutosha
iii. Khanga au kitenge doti moja tu
iv. Mwanafunzi anaweza kuja na nguo za kulalia (night dress)
v. Nguzo za ndani za kutosha

**N.B MUHIMU**

a. Mzazi/Mlezi wa mwanafunzi tafadhali zingatia vipimo hivyo, mwanafunzi atakayeshona na kuja na sketi/ shamba dress kinyume na vipimo, rangi na aina ya kitambaa tulichoelekeza hatapokelewa, zitarudishwa nyumbani ili aje na sare zilizoelekezwa.

b. Mwanafunzi anaweza kushona idadi ya sare kadri ya uwezo wake, ila anashauriwa awe na angalau sare jozi (pair) mbili za darasani.

c. Mwanafunzi anatakiwa kuvaa sare wakati wote wa masomo na anapokwenda hospitali, mjini au anapokuwa katika shughuli zote za kishule nje ya eneo la shule

d. Ni marufuku kabisa kujipamba wakati amevaa sare ya shule akiwa shuleni (make up)

e. Mwanafunzi haruhusiwi kuja na nguo za nyumbani.

## 1.3 MAHITAJI MENGINE MUHIMU KWA WANAFUNZI WOTE

i. Sanduku la bati linalofunga vizuri (trunck lenye kufuli mbili)
ii. Godoro la futi 3x6 kwa wasichana tu
iii. Godoro la futi $2^1/_2$ x 6 kwa wavulana tu
iv. Blanket moja la futi 3x6 (kwa wale wanaohitajia kuja nalo)
v. Aje na mto na foronya yake kulingana na rangi ya shuka
vi. Taulo za bafuni
vii. Kanda mbili kwa ajili ya kuogea
viii. Viatu vya plastic yebo kwa ajili ya kushindia.
ix. Chandarua/ neti futi 4x6 pande nne (**rangi ya blue**). **Ni muhimu na lazima kwa kila mwanfunzi kuwa na neti**
x. Bima ya afya, kama hana tunashauri umkatie bima ya afya kabla ya kuripoti.
xi. Aje na container lenye mfuniko/ sahani, bakuli, kikombe na kijiko.

## 1.4 MAHITAJI YA KITAALUMA

i. Madaftari counter book 10 QUIRE 3 au QUIRE 4.
ii. Pen, pencils,( mathematical set, scientific calculator na graph pad 1 kwa wanafunzi wa HGL na HGK),
iii. Ream A4 mbili kwa mwaka, kila muhula Ream Moja
iv. File mbili kwa ajili ya kutunzia majaribio na taarifa binafsi za mwanafunzi
v. Result slip ya kidato cha nne
vi. Nakala ya cheti cha kuzaliwa

## 1.5 VIFAA VYA USAFI

i. Tahasusi ya HGK waje na Jembe, fyekeo/ kwanja na squiezer.
ii. Tahasusi ya HGL waje na Reki, Panga na hard broom
iii. Tahasusi ya HKL- waje na soft broom, mopa na Panga
iv. Fagio ya chelewa kwa ajili ya usafi wa nje kwa wanafunzi wote
v. Ndoo ndogo mbili zenye mifuniko
vi. Sabuni ya **chooni lita tano** kwa wanafunzi wote.
vii. Dumu tupu la lita tano kuhifadhia maji ya kunywa.

**N.B MUHIMU** Mwanafunzi alete kifaa na sio pesa

## 2. MICHANGO MINGINE

| S/N | AINA YA MCHANGO | KIASI (tshs) |
|---|---|---|
| 1 | Mchango wa uendeshaji wa shule | 65,000/= |
| 2 | Tahadhari | 5,000/= |
| 3 | Nembo | 5,000/= |
| 4 | Kitambulisho cha shule | 5,000/= |
| **JUMLA** | | **80,000/=** |

**ZINGATIA:** Michango tajwa hapo juu ifanyike kupitia akaunti Namba **70201200065 NMB** jina la akaunti ni KITOMANGA SEKONDARI. Pesa taslim haitapokelewa hivyo mwanafunzi aje na pay-in slip

## 3.0 TAALUMA

Kila Mwanafunzi ni lazima ahudhurie vipindi vyote vya masomo na kufanya mazoezi yote anayopewa na mwalimu wa somo husika, pia na mitihani yote ndani na nje ya shule.

## 4.0 SHERIA NA KANUNI MUHIMU ZA SHULE.

Shule ya Sekondari Kitomanga inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria na miongozo iliyopo. Kila mwanafunzi anatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni.

### Sheria na Kanuni za Shule

i. Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.
ii. Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule;
iii. Kushiriki kwa kikamilifu masomo ya usiku(Preparation);
iv. Kuwahi katika kila shughuli za shule utakazopewa;
v. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo ya kuwepo ndani na nje ya,shule ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako
vi. Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule;
vii. Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa;
viii. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote;
ix. Kutunza mali za shule;
x. Ni marufuku mwanafunzi kumiliki vifaa vyenye ncha kali na dawa bila idhini
xi. Mwanafunzi haruhusiwi kubadili dini wala kumshawishi mwanafunzi mwenzake kubadili dini wawapo shuleni.

xii. Mwanafunzi hataruhusiwa kusuka nywele, wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na nywele fupi wakati wote wawapo shuleni.

**MUHIMU**

- Mwanafunzi hapaswi kuja na simu shuleni kwa namna yoyote ile, na hakuna mtumishi anayeruhusiwa kutunza simu ya mwanafunzi; Mawasiliano yote yafanyike kupitia mkuu wa shule.

- Mwanafunzi awapo shuleni atatakiwa kulala kwenye Bweni alilopangiwa na kitanda alichopangiwa. Ni marufuku mwanafunzi kulala kitanda kimoja na mwenzake au kuishi kwenye Bweni ambalo hakupangiwa.

- Mwanafunzi ataruhusiwa kurudi nyumbani kwa ruhusa na kibali maalum toka kwa Mkuu wa Shule. (Msiba au Ugonjwa).

## 5. 0. MAKOSA YATAKAYOSABABISHA MWANAFUNZI AFUKUZWE SHULE

i. Wizi;

ii. Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/utoro;

iii. Kugoma na kuhamasisha mgomo, kuongoza au kushiriki kuvuruga amani na usalama wa shule au watu

iv. Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/walezi na jamii kwa ujumla;

v. Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au mtu yeyote yule;

vi. Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya dawa za kulevya;

vii. Uvutaji wa sigara;

viii. Uasherati, mahusiano ya jinsi moja, kuoa au kuolewa;

ix. Kupata ujauzito au kutoa mimba au kusaidia vitendo vya kutoa mimba

x. Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi;

xi. Kwenda kwenye nyumba za starehe na nyumba za kulala wageni;

xii. Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule;

xiii. Kudharau Bendera ya Taifa;

xiv. Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu xv. Uharibifu wa mali ya umma kwa makusudi. xvi. Kudharau bendera ya Taifa na wimbo wa Taifa.

xvii. Kukataa/kudharau/kugomea adhabu halali iliyotolewa.

## 6.0. MAELEZO YA ZIADA KWA MZAZI/MLEZI

i. Shule inafuata mihula inayotolewa na Serikali. Mzazi /mlezi hakikisha mtoto anafika shuleni kwa wakati.
ii. Mawasiliano yoyote kati ya mwanafunzi na mzazi/mlezi yafanyike kupitia Mkuu wa shule, Makamu mkuu wa shule na ofisi ya Malezi.
iii. Shule itaruhusu wazazi kuwaona wanafunzi siku ya mapumziko katika juma la mwisho wa mwezi. Endapo atahitajika, mzazi ataitwa na uongozi wa shule.
iv. Aidha unashauriwa kutomruhusu mwanao kumiliki simu kipindi hiki ambacho umri wake unampa shida kuyatawala mazingira ya utandawazi.
v. Mzazi/mlezi kutompa mtoto fedha nyingi ambazo zitamfanya apoteze utulivu wa akili na kuvunja sheria za shule.
vi. Shule ina utaratibu wa kushughulikia usafiri kwa wanafunzi wanaotoka mbali kipindi shule inapofunga. Hivyo mzazi/mlezi utapewa taarifa na gharama za nauli kabla ya shule kufunga. vii. Mzazi hakikisha unapima afya ya mwanao kwa uaminifu ili kuepuka usumbufu wakati wa masomo.
viii. Iwapo mwanao ana ugonjwa unaomsumbua mara kwa mara, tafadhali aje na vyeti pamoja na dawa anazotumia na akabidhi kwa Muuguzi wa Shule. Tafadhali usifiche ugonjwa;
ix. Mwanafunzi anaruhusiwa kuja na pasi ya mkaa kwa ajili ya kunyooshea nguo zake. Ni marufuku mwanafunzi kutumia pasi ya umeme ama kifaa chochote kinachotumia umeme. Akibainika hatua kali zitachukuliwa dhidi yake ikiwemo kusimamishwa shule.
x. Shule itakapokuwa imefunga, mwanafunzi atatokea shuleni moja kwa moja kwenda kwa mzazi wake (nyumbani kwao) na shule itakapofunguliwa atatokea nyumbani kwao (kwa mzazi) kuja shuleni.

## 7.0 VIAMBATISHO NA FOMU MAALUM

i. Fomu ya Uchunguzi wa Afya (Medical Examination Form) ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa Hospitali ya Serikali;

ii. Fomu ya Maelezo Binafsi kuhusu Historia ya Mwanafunzi/Mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai;

iii. Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yanayotolewa shule; na

iv. Picha nne (4) za wazazi na ndugu wa karibu wa mwanafunzi wanaoweza kumtembelea mwanafunzi shuleni pamoja na Namba zao za Simu.

**8.0** Tafadhali soma kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.

**KARIBU SANA KITOMANGA SEKONDARI…!**

**NB:** ***KUMEKUWA NA UTAPELI (WIZI KWA NJIA YA MITANDAO KUPITIA UJUMBE MFUPI AU KUPIGIWA SIMU NA WATU WANAOJITAMBULISHA KAMA NI WALIMU).***

**TAFADHALI UPATAPO UJUMBE WOWOTE KUHUSU MWANAFUNZI/MTOTO WAKO USITUME CHOCHOTE. PATA UKWELI WA TAARIFA HUSIKA KUTOKA KWA UONGOZI WA SHULE KWA NAMBA ZIFUATAZO**

- **Mkuu wa Shule: 0786763078**
- **Makamu Mkuu wa Shule: 0685128372**

***SCHOOL MOTTO: ELIMU NI UFUNGUO WA MAISHA***

**FOMU NAMBA 1**

**KUKUBALI AU KUKATAA NAFASI YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KWA MWAKA 2026.**

Mimi ……………………………………………………….………… nakutaarifu kuwa nimepokea barua ya kuchaguliwa kujiunga na Shule ya Sekondari Kitomanga. NIMEKUBALI/ NIMEKATAA nafasi hii baada ya kusoma na kuelewa yaliyoandikwa katika fomu na barua ya kujiunga.

Ninaahidi mbele ya Mzazi/Mlezi wangu kuwa nikishafika shuleni, nitazingatia kanuni,,sheria na taratibu zote za shule kwa kipindi chote cha mimi kuwa mwanafunzi wa Shule ya Sekondari Kitomanga. Na nimeelewa kanuni na taratibu zote za shule na sitajihusisha na vitendo vya uvunjaji wa amani shuleni, kushiriki kufanya fujo, vurugu, migomo, kuvuta bangi na matumizi ya madawa ya kulevya pamoja na makosa ya jinai. Nitatumia juhudi na maarifa katika kujiendeleza kwa manufaa yangu na Taifa kwa ujumla.

Jina la mwanafunzi ………………………………………………………….……………………

Saini……………………………………….

Tarehe…………………………………..….

**FOMU NAMBA 2**

**MEDICAL EXAMINATION FORM**
**PRESIDENT'S OFFICE**
**REGIONAL ADMINISTRATION AND LOCAL GOVERNMENT**

Kitomanga Secondary School,

P.O BOX 464,

LINDI.

**REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION.**

Please examine Miss/Mr ........................................................................................ as his/her physical and Mental fitness for admission as a form …………………….. Students at Kitomanga Secondary School in the year ……………… Your sincerely.

BAHIA T. ABUBAKAR

HEADMISTRESS

MKUU WA SHULE
KITOMANGA SEKONDARI
LINDI

The headmistress,

I have examined Miss/Mr.………………………………………………………..

Shown and consider that he/she is physically and mentally fit/unfit for admission to pursue a full-time advanced secondary school course.

1. Vision with/without glasses. Right ………… Left ……………….
2. Blood pressure …………………………… Hemoglobin ………………………
3. Hearing ………………………………………………………
4. Urine (a) Albumen ………………………… (b)...........................
5. a) Venereal diseases………………… (b) Bilharzia............................
6. Pregnancy …………………………………………………………
7. Neurosis……………………………………………………………
8. Is there any abnormality of: (a) the heart…………………………….

b) Lungs ……………………… c) The spleen …………………

1. Are there serious diseases. E.g. Leprosy, Epilepsy, Asthma, Diabetes, etc.
……………………………………………………………………………..

Date ……………………………Signature of the medical Officer……………………………….

Station ………………………… Designation ……………………

**FOMU NAMBA 3**

**TAARIFA ZA ANAKOTOKA MWANAFUNZI**

1. Mkoa ………………………………….. Wilaya …………………………………………
2. Tarafa …………………………… Kata ……………………………………………..
3. Mtaa/Kijiji ……………………………………………
4. Jina la Mtendaji wa Kijiji/Mtaa ……………………………..………….Saini………………….

Tarehe………………………………. Mhuri……………………………. Simu…………………...

5. Michezo anayopendelea mwanafunzi.

| SN | Jina la mchezo |
|---|---|
| | |
| | |
| | |
| | |
| | |

9. Nafasi yoyote ya uongozi aliyowahi kushika

| NS | Aina ya uongozi | Shule | Mwaka |
|---|---|---|---|
| | | | |
| | | | |
| | | | |

Nathibitisha kwamba taarifa nilizozitoa hapo juu ni za kweli, pia nathibitisha kuwa nitakuwa na tabia nzuri, mchapa kazi pamoja na kuwa na bidii ya masomo

NB: Pamoja na fomu hizi ambatanisha na kopi ya cheti cha kuzaliwa na nakala halisi ya matokeo. (Result slip)

Jina la Mwanafunzi ………………………….. ….Saini ………………… Tarehe ……………

**FOMU NAMBA 4**

**TAARIFA ZA MZAZI/MLEZI**

1. Jina kamili la Mzazi/Mlezi ……………………………………………….

2. Kazi anayofanya mzazi …………………………………………………

3. Anuani ……………………………………………………….

4. Namba ya simu …………………………………….

5. Mkoa ……………………. Wilaya ……………… Tarafa ………………… Kata ……………………………… Kijiji ……………………. Mtaa ……………

1. Anuani kamili ya nyumbani ambako mwanafunzi atakuwa anakwenda wakati wa likizo

Mahali ……………………………………. kwa nani ……………………

**Majina ya viongozi/Wazazi /walezi atakakokuwa anakwenda wakati wa likizo**

Jina la Baba /mlezi/ndugu ………………………………………..

Jina la mama/mlezi ……………………………………………….

Mtendaji wa Kata …………………………………………  Mtendaji wa Kijiji/Mtaa ……………………………………….……

Mwenyekiti wa Kijiji/Mtaa …………………………………………….

**FOMU NAMBA 5**

**NDUGU WA KARIBU WA MWANAFUNZI**

Ndugu wa karibu na mwanafunzi: Hakikisha unaandika majina matatu na anwani zao. Hii inasaidia shule kutoa taarifa endapo tatizo litatokea.

(**Bandika passport size kwa kila ndugu kwenye kisanduku kilixchopo upande wa kulia)**

1. (a) Jina: ___________________________________

(b) Uhusiano: _________________________________

(c) Anwani: __________________________________

(d) Namba ya Simu: ___________________________

2. (a) Jina: __________________________________

(b) Uhusiano: ________________________________

(c) Anwani: _________________________________

(d) Namba ya Simu: ___________________________

3. (a) Jina: __________________________________

(b) Uhusiano: ______________________________

(c) Anwani: ________________________________

(d) Namba ya Simu: _________________________

4. (a) Jina: _________________________________

(b) Uhusiano: ____________________________

(c) Anwani: ______________________________

(d) Namba ya Simu: _______________________

Saini ya mzazi ________________________________
Tarehe:________________

**FOMU NAMBA 6**

**TAMKO LA MZAZI/ MLEZI**

Mimi Mzazi/Mlezi wa ………………………………………………. Ninaahidi kushirikiana na walimu pamoja na watumishi wote wa Shule ya Sekondari Kitomanga katika kumlea mwanangu kwa muda wote atakapokuwa shuleni.

Nitaomba kujulishwa mara moja endapo mwanangu ameenda kinyume na sheria, kanuni na taratibu za shule. Pia nitakuwa tayari mwanangu kupewa adhabu inayostahili kwa makosa atakayofanya. Ikiwa ni pamoja na kufukuzwa shule pale itakapobidi.

**Jina la Mzazi/Mlezi ………………………………………………………..………….**

**Sahihi ……..........................................……**

**Tarehe ……………………………………….**

## ORODHA YA VITABU MUHIMU KWA MWANAFUNZI

### ENGLISH LANGUAGE

1. English Language for Advanced secondary schools student’s Book Form Five by TIE. Tanzania Institute of Education Publishers.
2. English. for Advanced level by Dr. M. Kadeghe
3. Advanced English Dictionary –Oxford University
4. Poets of Africa: Lament of the Silent & Other Poems (2024) by Jared Angira. East Africa Educational Publishers Ltd.
5. Summons: Poems from Tanzania (2023) by Richard S. Mabala et al. Mkuki na Nyota publishers Ltd
6. Animal Farm by George Orwell (2023). East Africa Educational Publishers Ltd
7. Chasing the Leopard Finding the Lion by Julie Wakeman Linn (2024). Mkuki na Nyota publishers Ltd
8. The opportunist Elite by Nyambari C. M Nyangwine (2023). Mbesa Books Distributors.
9. The horizon Unveiled by Fellowes Mwaisela (2011). FGD Tanzania Ltd
10. The Government Inspector by Nikolai V. Gogol (2024). East Africa Educational Publishers Ltd.
11. A Taste of Heaven by Farouk Topan (2023). Mkuki na Nyota Publishers Ltd
12. An Enemy of the People by Henrik Ibsen (2024). East Africa Educational Publishers Ltd
13. Competence in advanced level English language form five 2025 by Imani Simoni Milanzi
14. Competence in linguistics advanced level form five 2025 by Mgonja, M.E

### ACADEMIC COMMUNICATIO.

1. Academic communication for Advanced Secondary Schools Student’s Book Form Five (2024) by Tanzania Institute of Education. TIE Publishers.
2. Academic communication Questions with Answer review Form Five by Mgonja, M.E

### KISWAHILI

1. Kiswahili Shule za Sekondari kitabu cha mwanafunzi kidato cha tano (2024) –Taasisi ya Elimu Tanzania
2. Sarufi ya Kiswahili Sekondari na Vyuo (Mdee) DUP-DSM
3. Kamusi ya Kiswahili Sanifu – TUKI.
4. Sarufi maumbo ya Kiswahili sanifu (SAMAKISA) sekondari na vyuo (2009) na Masamba na wenzake
5. Dunia uwanja wa Fujo- Euphrase Kezilahabi (2023). Africa Proper Education Network
6. Ua la Faraja-W.E Mkufya (2007). Mangrove Publishers
7. Mirathi ya Hatari-C.G. Mung’ong’o (2023). Mkuki na Nyota Publishers Ltd
8. Wasifu wa Siti binti Saad- Shaaban Robert (2023). Mkuki na Nyota Publishers Ltd
9. Mukwawa wa Uhehe-M.M. Mulokozi (2023). Africa Proper Education Network
10. Malenga wa Ziwa Kuu-wallah Bin Wallah (2024). East Africa Educational Publishers Ltd

11. Andamo, Msafiri Safarini-Mohammed Khelef Ghassani (2023). Educational Books Publishers Ltd
12. Wosia wa Baba- Ahmed Mohamed Amanzy (2024). Abantu Publication Ltd.

**GEOGRAPHY**

1. Physical Geography for Advanced Secondary Schools Student's Book Form Five and Six (2024) by Tanzania Institute of Education. TIE Publishers.
2. Practical Geography for Advanced Secondary Schools Student's Book Form Five and Six (2024) by Tanzania Institute of Education. TIE Publishers.
3. Physical Geography in diagram 4th edition by R. B. Bunnett

**HISTORY**

1. History for Advanced Secondary Schools student's Book Form Five (2024) by TIE, Tanzania Institute of Education Publishers.
2. Bakari Madaya (2025). *History for high schools form five.* Bisha's Modern Printers.
3. Magoti Bernard (2025). *The Ultimate Principles of History one form five.* Matokeo Publishers and Printers.

**HISTORIA YA TANZANIA NA MAADILI**

1. Historia ya Tanzania na Maadili shule za sekondari kitabu cha mwanafunzi, kidato cha Tano (2024). Taasisi ya Elimu Tanzania.

**VIELELEZO VYA PICHA KUHUSU UNIFORM/SARE**



KITAMBAA CHA SARE YA DARASANI KWA WOTE



TRACK SUIT






JEZI KWA WASICHANA

JEZI KWA WAVULANA